**HOTUBA YA MHESHIMIWA MAJ. GEN (mst) SALUM MUSTAFA KIJUU, MKUU WA MKOA WA KAGERA, KATIKA SHEREHE YA SIKUKUU YA MEI, MOSI, 2017, KIMKOA KATIKA VIWANJA VYA MASHUJAA MANISPAA YA BUKOBA 1/5/2017**

Mwenyekiti wa TUCTA Mkoa wa Kagera,

Katibu Tawala Mkoa,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Bukoba,

Waheshimiwa Wabunge,

Mheshimiwa Meya,

Wenyeviti na Makatibu wa Vyama vya Wafanyakazi;

Waheshimiwa Wenyeviti na Makatibu wa Vyama vya Siasa;

Waheshimiwa Viongozi wa Serikali;

Waheshimiwa Viongozi wa Madhehebu ya Dini;

Waheshimiwa Viongozi wa Taasisi mbalimbali Mkoani Kagera;

Ndugu Wafanyakazi na Wananchi;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana.

Itifaki imezingatiwa.

***Kagera…………….Kazi Amani na Maendeleo.***

***Kazi, Amani na Maendeleo………….Kagera.***

**"UCHUMI NA VIWANDA" ULENGE KULINDA HAKI, MASLAHI NA HESHIMA YA WAFANYAKAZI**

Mhe. Mwenyekiti wa TUCTA Mkoa, Viongozi wa Chama na Serikali na Ndugu Wafanyakazi mliopo hapa, naomba tuungane kwa pamoja kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa kwenye tukio hili muhimu la Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wafanyakazi kwa mwaka 2017.

Kipekee sana niwashukuru Viongozi wa TUCTA na Wafanyakazi kwa ujumla Mkoani Kagera kwa kunialika kuungana na Wafanyakazi wenzangu kuadhimisha siku hii adhimu na ya Kihistoria, niwashukuru pia Mhe. Mkuu wa Wilaya ya bukoba na Meya wa

Manispaa kwa niaba ya Wananchi wa Manispaa hii kwa kutupokea vizuri tangu tulipowasili katika viwanja hivi vya mashujaa.
**Asanteni Sana.**

Ndugu Viongozi, kuandaa sherehe kubwa kama hii sio kazi rahisi, tuungane sote kuwatia moyo vyama shiriki vya TUCTA kwa maandalizi, nafahamu katika kipindi hiki ambacho Serikali ya awamu ya Tano ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Dr. John Pombe Joseph Magufuli, ya HAPA KAZI TU, na kubana matumizi, Inawezekana kabisa mkawa mmekabiliana na changamoto katika kupata ushiriki wa ari na mali toka kwa wadau wenu mbalimbali, ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Kwa niaba ya wafanyakazi wote katika mkoa huu naomba mpokee shukrani zetu nyingi kwa kazi nzuri mliyofanya hasa kwa kuendana na dhana ya kubana matumizi.

***Ndugu Wafanyakazi*,**
Kwa namna ya pekee nitoe pongezi zangu kwenu nyote wafanyakazi katika mkoa wa Kagera kwa kutekeleza majukumu yenu katika mwaka mzima kwa mafanikio makubwa ambayo yanaonekana. Nakiri kwamba ufanisi wenu mzuri wa kazi umeupatia mkoa mafanikio mazuri katika nyanja mbalimbali.

Aidha, nizidi kuwapongeza kwa kusherekea salama miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioanzishwa na waasisi wetu Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na Abeid Amani Karume mwaka 1964. Nawasihi tuzidi kuuenzi. ***Muungano ….. Daima.***

***Umuhimu wa Siku ya Wafanyakazi Duniani***
Kwa namna ya pekee nawapongeza sana wafanyakazi wote mkoani Kagera kwa kuadhimisha siku hii. Ni siku ambayo wafanyakazi duniani kote wanakumbushana umuhimu wa mshikamano na umoja katika kudai na kutetea maslahi na maendeleo yao. Ni siku wafanyakazi wanaungana pamoja kutafakari jinsi mnavyotimiza wajibu wenu wa kutoa huduma na kuzalisha mali pamoja na kutambua changamoto zinazowakabili na kuweka mikakati ya kuzikabili.

***Pongezi kwa Wafanyakazi Bora***

***Ndugu Wafanyakazi;***

Nawapongeza wafanyakazi wote mliopewa tuzo ya kuwa wafanyakazi bora katika sehemu zenu za kazi. Hongereni sana kwa mafanikio haya. Nina uhakika kwamba wapo wafanyakazi wengine wengi ambao wanafanya kazi kwa bidii katika maeneo yenu ya kazi lakini hawakubahatika kupata tuzo. Niwaombe msikate tamaa, muendelee kuchapa kazi. Huenda mkabahatika kupata Mei Mosi ijayo. Napenda kuwakumbusha kauli mbiu ya Mhe. Rais ya HAPA KAZI TU, chapeni kazi kwa bidii, umahiri, weledi, kwa kasi inayohitajika ili kupunguza malalamiko toka kwa wateja wenu, tukibadilika sote katika utoaji wa huduma, Mahospitali, Mashuleni. Viwandani, Mahotelini, ofisi za umma na hata ofisi binafsi, tutakuwa tumejibu kiu ya watanzania na kuendana na kauli mbiu ya HAPA KAZI TU.

***Kauli Mbiu ya Mwaka huu***
***Ndugu Wafanyakazi*,**

Naomba niwakumbushe Kauli Mbiu ya Sherehe za Mwaka huu isemayo "UCHUMI WA VIWANDA ULENGE KULINDA HAKI, MASLAHI NA HESHIMA YA WAFANYAKAZI"

Ni Kauli Mbiu yenye ujumbe maridhwa ambao umekuja wakati muafaka kabisa. Kwanza ni kwa sababu katika awamu ya Tano ya Serikali ya awamu ya Tano, Maendeleo yake yako " Centred" kwenye dhana ya Viwanda, hii ni kutokana na Ilani ya chama Tawala 2015 na kwa Mujibu wa Maelekezo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania.

Binafsi na kwa nafasi yangu kama Kiongozi wenu wa Mkoa nakubaliana na Maudhui ya Kauli Mbiu hiyo kwamba "Uchumi wa Viwanda Ulenge Kulinda haki, maslahi na heshima ya Wafanyakazi". Ni ushahidi usiohitaji tafiti za Kisayansi kuwa uchumi huo wa Viwanda tunaotegemea hautafanikiwa iwapo kauli mbiu hii itapuuzwa, kwani uchumi wa Viwanda unahitaji wataalam ambao ni sehemu ya wafanyakazi tunaoadhimisha siku yetu muhimu leo hapa. Hivyo ni Wito wangu kwa Viongozi wenzangu ngazi zote katika Mkoa wetu wa Kagera wanaosimamia watumishi, kuhakikisha kuwa haki, maslahi na heshima ya wafanyakazi wa ngazi zote yanalindwa, na kwa wale wanaosimamia maslahi na heshima ya Wafanyakazi, TUCTA ikiwemo kuhakikisha mnakuwa bega kwa

bega na Mamlaka za Serikali na mashirika binafsi ili kusimamia na kutetea haki hizo kwa ngazi zote bila uwoga.

Aidha ni wito wangu kwenu wafanyakazi wenzangu kukumbuka kuwa haki na heshima ya Mfanyakazi inapatikana kwa kutimiza Wajibu wenu katika nafasi zetu za Kiutendaji na Kiuongozi. **TUTIMIZE WAJIBU WETU**.

Mhe. Mwenyekiti na Wafanyakazi Wenzangu, hivi punde nimesikia risala yenu ilioyosomwa kwa niaba ya wafanyakazi wote. Naomba kwa ruhusa yenu niweze kutoa ufafanuzi wa masuala yaliyoelezwa kwenye risala.

***Kuhusu Maslahi mbalimbali ya Wafanyakazi:-***

Mhe. Mwenyekiti na Wafanyakazi Wote, Ni ukweli kuwa lengo la la Serikali ni kuendelea kuboresha maslahi ya Wafanyakazi hasa mishahara kwa sekta zote, miongoni mwa mambo yaliyofanywa na Serikali katika kuboresha maslahi ya watumishi ni pamoja na kutungwa kwa Sera mpya na malipo ya mishahara na motisha kwa Utumishi wa Umma na kuundwa kwa bodi ya Mishahara katika utumishi wa Umma. Kadhalika Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na ukuaji wa Uchumi.

Napenda kupitia Sherehe hizi, kama nilivyosema mwaka jana kwenye tukio kama hili, kuwaomba wafanyakazi wote kufanya kazi kwa bidii, kulipa kodi mbalimbali kwa uaminifu mkubwa, kudai risiti pale unaponunua bidhaa na kutoa taarifa kwa wale wote wanaokwepa kulipa kodi, tukifanya mambo hayo tutasaidia Serikali yetu kuongeza mapato na hivyo kuboresha mishahara na maslahi mengine ya Watumishi wa Umma, hali kadhalika tulioko sekta binafsi ni wito wangu kwenu kuongeza bidii katika maeneo yenu ya kazi ili kuongeza uzalishaji na faida kwa mwajiri ili maslahi na haki za mtumishi kama Kaulimbiu ya Mwaka huu inavyotuasa, ziweze pia kuboreshwa.

***Kuhusu Mikataba kwa Wafanyakazi***:-

Mhe. Mwenyekiti Mikataba ya kazi kwa Mfanyakazi ni matakwa ya kisheria. Sheria ya Mahusiano kazini, Sheria No. 6/2004 kwa mujibu wa fungu la 14 likisomwa pamoja na

fungu namba 15 linamwagiza kila Mwajiri kuwa na Mkataba baina yake na Mwajiriwa na Mkataba huu ni sharti kukidhi matakwa ya Kisheria

Mhe. Mwenyekiti wa TUCTA na Wafanyakazi wote, kwa maana ya vifungu hivi vya sheria, mwajiri analazimika kisheria kumpa mtumishi Mkataba kuwa sio zawadi au matakwa ya Mwajiri, kwa kuwa Sheria inatumia neno "shall" sio “Option ni Madatory"

Mhe. Mwenyekiti mwaka jana kwenye jambo hili lilielezwa katika risala yenu, na katika majibu yangu nilisema jambo hili sio la kusubiri kusemwa siku ya maadhimisho kama haya, Ofisi yangu na Katibu Tawala wa Mkoa iko wazi siku zote, na ninaamini pia Ofisi zenu TUCTA na Washirika wenu mko kazini siku zote, leteni taarifa hizi ili zishughulikiwe, zikiwa na Waajiri "Specific" ambao wanakwenda kinyume na matakwa ya sheria hii muhimu.

***Kuhusu Unyanyasaji wa Wafanyakazi Mahali pa Kazi***

Mhe. Mwenyekti wa TUCTA Mkoa, katika risala yenu lipo jambo kuhusu wafanyakazi kunyanyaswa, kudhulumiwa haki zao, kufukuzwa kazi ovyo, matendo yanayofanywa na baadhi wa Wasimamizi wa kazi katika Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

Usimamizi wa Wafanyakazi katika nchi yetu umewekewa utaratibu, ni mategemeo yangu TUCTA na washirika wenu mnazifahamu taratibu hizi zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria. Imeelezwa katika risala yenu kuwa Sekta binafsi hususani, Mahotel, Makampuni ya Ulinzi yanaongoza katika hili. Bado wito wangu kwako Mhe. Mwenyekiti wa TUCTA na washirika wako, leteni majina ya Taasisi hizi, pamoja na "Specific cases" ili ofisi yangu kwa kushirikiana na wasimamizi wa Wafanyakazi waweze kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria.

Kuhusu Malimbikizo ya Madai mbalimbali ya Watumishi Mhe. Mwenyekiti wa TUCTA MKOA na wafanyakazi Wote Serikali ya awamu ya tano imeweka utaratibu wa kulipa madeni ya ndani na nje kila mwezi ikiwemo deni la PSPF na NSSF, hali hii imedhihirika sasa kutokana na Wastafu kuanza kulipwa mafao yao. Nawashauri Watumishi wote wanaotarajia kustaafu hivi karibuni kuendelea kutoa taarifa ya kustaafu kwao ndani ya muda unaotakiwa pamoja na kuhakikisha nyaraka zote zinazohusiana na hitimisho la

kazi zinakuwepo ili kurahisisha malipo yao ya mafao yanafanyika bila kikwazo cha kukosekana kwa nyaraka.

Mhe. Mwenyekiti kuhusu baadhi ya Watumishi wa Umma kunyagan'ywa vyeo baada kupandishwa kama ilivyoelezwa kwenye risala yenu, watumishi hao walioondolewa vyeo vyao kutokana na zoezi la uhakiki wa watumishi lililokuwa linaendelea Muda si mrefu zoezi hili litahitimishwa.

**Kuhusu kuitishwa mabaraza ya wafanyakazi**

**Mhe mwenyekiti wa mkoa**

Ni kweli sheria No. 19 ya mwaka 2003 inatoa wajibu kwa waajiri kutopitisha bajeti za taasisi zao pasipo kuitisha baraza la Wafanyakazi mahali pa kazi. Risala yenu inayonesha Halmashauri za Bukoba Vijijini, Ngara na Biharamulo zimekuwa sugu kwenye jambo hili. Ni maelekezo yangu kwa Katibu Tawala wa Mkoa, kuhakikisha kuwa katika mwaka wa fedha ujao 2018/2019 hakuna halmashauri ambayo bajeti yake itajadiliwa katika ngazi ya Mkoa iwapo haitakuwa imepitiwa na Mabaraza ya Wafanyakazi.

Ndugu, Wafanyakazi wenzangu Serikali ya awamu ya Tano inawathamini sana inawezekana katika kipindi hiki cha mwanzo wa awamu hii, Jambo hili lisieleweke sana. Hata hivyo ni maombi yangu kwenu kuendelea kuomba uzima na Kuiombea Serikali yetu na Viongozi wake ili mema ya nchi yanayopangwa na awamu hii tuyashuhudie. Katika kuthibitisha jambo hili  Serikali imetoa kiasi cha fedha Tshs. 239,192,659/= ikiwa ni sehemu ya madeni ya Walimu katika Halmashauri zetu saba Mkoani hapa, kwa hapa Manispaa zimetengwa Tshs. 23,000,000/ Bukoba Vijijini 36,934,000/=, karagwe Tshs. 40,700,000/=, ngara Tshs. 10,031,000/= Kyerwa Tshs. 39,889,679.00, Missenyi Tshs. 52,952,680/= na Muleba Tshs. 20,792,800/=.

Fedha hizi ziko hatua mbalimbali za malipo katika halmashauri zetu. Niwaombe walimu watakaonufaika na malipo haya kuzitumia vizuri kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya kujiongezea kipato katika ngazi za Kaya.

Mhe. Mwenyekiti wa TUCTA Mkoa na Wafanyakazi wenzangu yapo malalamiko ya mikataba ya Wafanyakazi kwa watumishi hususani sekta binafsi, lakini pia kuzuiwa kwa shughuli za Vyama vya Wafanyakazi katika baadhi ya Ofisi mnazozitumikia.

Kwa kuwa mambo haya yapo kwenye sheria ya ajira na mahusiano kazini ya mwaka 2006, kifungu cha 9(i), na mimi na wenzangu kazi yetu, ni pamoja na kusimamia sheria na taratibu zilizopo, niwaombe sana Viongozi wa TUCTA, taasisi hizo zinazokiuka sheria za nchi, hazipaswi kuvumiliwa hata kidogo. Wito wangu kwa Wasimamizi wenzangu ngazi mbalimbali msiwafumbie macho waajiri wa namna hii.

Wafanyakazi ndio Msingi wa Maendeleo yote yanayozungumzwa, kuanzia kwenye Ilani, matamko, miongozo na dira mbalimbali za Serikali ili kufanikiwa katika maendeleo ya aina yoyote msingi wake ni kuwa na watumishi wenye weledi na wenye kujituma, ili waoneshe weledi na kujituma, Wafanyakzi hawa ni lazima tusimamie haki, maslahi na heshima yao ndipo Maendeleo ya Viwanda yatakuwa halisi.

Mhe. Mwenyekiti na Wafanyakazi wote, naomba sasa nitumie fursa hii kumaliza hotuba yangu kwa kuwashukuru na kuwapongeza kwa kutambua kwenu jitihadi za Serikali yetu pendwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

Niseme tu ofisi yangu iko wazi muda wote katika kujadiliana kwa pamoja namna ya kutatua changamoto za wafanyakazi zilizo ndani ya mamlaka yangu.

Nawasihi Watumishi wote Mahospitali, Mashuleni, vyombo vya Usalama, Sehemu zingine za kutoa haki kwa Wananchi, ziendelee kwa kutenda haki ili kujibu Kauli mbiu ya Mwaka huu ya MEI MOSI endeleeni kuwatumikia wananchi wetu bila ubaguzi, bila uonevu, bila ucheleweshaji wa makusudi, lakini ziadi sana wekeni utu mbele na utaifa, Daima kumbukeni, wewe leo mtumishi kesho utakuwa Mstaafu ama Mwananchi wa kawaida, ambae ungehitaji uhudumiwe kwa haki na heshima.. Hivyo tuwahudumie Wananchi wetu tukikumbuka kesho inakuja usiojua. Mhe. Mwenyekiti na Wafanyakazi wote niwatakie tena maadhimisho mema

Asante kwa kunisikiliza.

***Kagera…………….Kazi Amani na Maendeleo.***